TANGAZO LA SERIKALI NA. 383 la tarehe 17/05/2024

SHERIA YA USAFIRISHAJI MAJINI
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 376 (2) na 427)*

KANUNI ZA KUZUIA UCHAFUZI UNAOTOKANA NA MAJI TAKA KUTOKA KWENYE MELI ZA MWAKA 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Rejea inayofanana.

SEHEMU YA PILI
UTIRIRISHAJI WA MAJI TAKA

5. Katazo la utiririshaji wa majitaka.

SEHEMU YA TATU
VIFAA NA UDHIBITI WA UTIRIRISHAJI

6. Mifumo ya majitaka.
7. Viunganisho vya umwagaji.

## SEHEMU YA NNE
## UKAGUZI NA UTHIBITISHAJI WA MELI

8. Ukaguzi
9. Utoaji au uidhinishaji wa Cheti.
10. Utoaji au uidhinishaji wa Cheti na nchi nyingine mwanachama.
11. Utoaji au uidhinishaji wa Cheti cha serikali nyingine.
12. Muundo wa Cheti.
13. Muda na uhalali wa Cheti.
14. Katazo kwa meli ya Tanzania kufanya safari bila Cheti cha Majitaka.
15. Katazo kwa meli isiyo ya Tanzania kuingia baharini.
16. Majukumu ya mmiliki na nahodha wa meli ya Tanzania.
17. Masharti mengineyo kuhusiana na Cheti cha Majitaka.

## SEHEMU YA TANO
## UTEKELEZAJI

18. Ukaguzi wa meli.
19. Masharti ya kushikiria meli.
20. Mamlaka ya Mkuu wa Bandari kushikilia meli.
21. Wajibu wa Mkuu wa Bandari kutoa taarifa ya meli yenye upungufu.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

22. Makosa na adhabu.
23. Adhabu ya jumla.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA

24. Ushughulikiaji wa malalamiko.
25. Tathmini na utoaji taarifa.

**MAJEDWALI**

SHERIA YA USAFIRISHAJI MAJINI
(SURA YA 165)

**KANUNI**

*((Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 376 (2) na 427)*

KANUNI ZA KUZUIA UCHAFUZI UNAOTOKANA NA MAJI TAKA KUTOKA KWENYE MELI ZA MWAKA 2024

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Kuzuia Uchafuzi Unaotokana na Maji Taka Kutoka kwenye Meli za Mwaka 2024.

Matumizi

**2**.-(1) Kanuni hizi zitatumika katika kutekeleza Kiambatisho cha IV cha Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi Unaotokana na Meli wa mwaka 1973, kama ulivyorekebishwa na Itifaki ya mwaka 1978.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) na kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3), Kanuni hizi zitatumika kwa-

(a) meli ya Tanzania ya 400GT, popote itakapokua, inayojihusisha na safari za kimataifa;

(b) meli ya Tanzania inayofanya kazi katika maji ya ukanada wa ncha za dunia;

(c) meli yoyote ambayo si ya Tanzania ya 400GT ikiwa ndani ya maji ya Jamhuri ya Muungano au maji yanayodhibitiwa na inayojihusisha na safari za kimataifa; na

(d) meli yenye ukubwa chini ya 400GT ambayo imethibitishwa kubeba zaidi ya watu 15;

(3) Kanuni hizi hazitatumika kwa-

(a) meli ya kivita;

(b) meli za usaidizi wa kivita;

(c) meli nyingine inayomilikiwa au kuendeshwa na Serikali na kutumika, kwa wakati huo, kwa huduma zisizo za kibiashara za Serikali; au

(d) meli ya 400GT ambayo inabeba zaidi ya watu 15.

Tafsiri

**3.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"abiria" maana yake ni mtu yeyote aliyebebwa melini isipokuwa-

(a) mtu aliyeajiriwa au anayehusika katika nafasi yoyote katika shughuli za meli;

(b) mtu aliye kwenye meli ama kwa mujibu wa jukumu la nahodha la kubeba watu waliokuwa kwenye meli iliyoharibika, walio hatarini au watu wengine, au kwa sababu ya hali nyingine yoyote ambayo nahodha, mmiliki au mkodishwaji, kama yupo, asingeweza kuzuia au kuchukua hatua za kuzuia kutokea kwa hali hiyo; na

(c) mtoto wa umri wa chini ya mwaka mmoja;

"bahari" inajumuisha mlango au mkondo wa bahari;

"Cheti cha Majitaka" maana yake ni Cheti cha Kimataifa cha Kuzuia Uchafuzi Unaotokana na Majitaka;

"eneo maalumu" maana yake ni eneo la bahari ambalo, kwa sababu za kitaalamu zinazotambulika kuhusiana na hali ya bahari, ikolojia na tabia mahususi ya idadi ya vyombo vya majini, matumizi ya mbinu maalumu yanahitajika kwa ajili ya kuzuia uchafuzi wa bahari kwa njia ya majitaka;

"IMO" maana yake ni Shirika la Bahari Duniani;

TS Na. 196 la 2005

"GT" maana yake ni ukubwa wa jumla wa meli ulioamuriwa kwa mujibu wa Kanuni zaUkubwa za Usafirishaji Majini;

"kanuni za eneo la ncha za dunia" maana yake ni Kanuni za Kimataifa za Meli zinazofanya kazi katika maji ya ukanda wa ncha za dunia, kama ilivyofafanuliwa chini ya kanuni ya XIV/1.1 ya SOLAS;

"Kiambatisho cha IV" maana yake ni Kiambatisho cha IV cha Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi Utokanao na Meli wa Mwaka 1973 kama ulivyorekebishwa;

"kituo cha baharini" maana yake ni usimikaji ulio mbali na ufukwe, ambapo shehena kichele, kimiminika au gesi, huhamishwa kati ya meli na meli kwa-

(a) kupakiwa kwenye meli baada ya kusafirishwa kutoka ufukweni; au

(b) kupakuliwa kutoka kwenye meli kwa ajili ya kusafirishwa hadi ufukweni;

"kutoka ardhi ya karibu" maana yake ni kutoka mpaka ambapo eneo la bahari la mamlaka inayohusika imeanzishwa kwa mujibu wa sheria ya kimataifa, isipokuwa, kwa madhumuni ya Mkataba "kutoka ardhi ya

karibu" mbali na kaskazini-mashariki ya pwani ya Australia itamaanisha kutoka kwenye mstari uliochorwa kutoka sehemu ya pwani ya Australia katika latitudo 11°00' KUS, longitudo 142°08' MAS hadi hatua katika latitudo 10°35' KUS, longitudo 141°55' MAS, kutoka hapo hadi latitudo 10°00' KUS, longitudo 142°00' MAS, kutoka hapo hadi latitudo ya uhakika 9°10' KUS, longitudo 143°52' MAS, kutoka hapo hadi latitudo 9°00' KUS, longitudo 144°30' MAS, kutoka hapo hadi latitudo 10°41' KUS, longitudo 145°00' MAS, kutoka hapo hadi latitudo 13°00' KUS, longitudo 145°00' MAS, kutoka hapo hadi latitudo 15°00' KUS, longitudo 146°00' MAS, kutoka hapo hadi latitudo 17°30' KUS, longitudo 147°00' MAS, kutoka hapo hadi latitudo ya uhakika 21°00' KUS, longitudo 152°55' MAS, kutoka hapo hadi latitudo 24°30' KUS, longitudo 154°00' MAS, kutoka hapo hadi kwenye pwani ya Australia katika latitudo 24°42' KUS, longitudo 153°15' MAS;

"maili ya baharini" maana yake ni maili ya baharini ya kimataifa ya mita 1,852;

"maji yanayodhibitiwa" maana yake ni maeneo ya maji ya bahari ambayo mamlaka na haki za Jamhuri ya Muungano zinatekelezwa kwa mujibu wa Sehemu ya XII ya Mkataba wa UNCLOS;

"maji ya ukanda wa ncha za dunia" maana yake ni maji ya Aktiki au eneo la Antaktika, kama ilivyotafsiriwa katika aya ya 2 hadi 4 ya kanuni ya 1 ya Sura ya XIV (XIV/1.2 hadi XIV/1.4) ya SOLAS;

"majitaka" maana yake ni-

(a) mifereji ya majitaka na uchafu mwingine kutoka kwa aina yoyote ya vyoo;

(b) mifereji ya majitaka kutoka kwenye majengo ya matibabu ikijumuisha zahanati, vituo vya wagonjwa kupitia sehemu ya kunawia, beseni za kunawia na matundu ya kutolea maji yaliyopo katika majengo hayo;

(c) mifereji ya majitaka kutoka kwenye maeneo yenye wanyama; au

(d) maji machafu mengine yakichanganyikana na majitaka yaliyorejewa kwenye aya (a), (b) na (c);

"maji ya Tanzania" maana yake ni ni kama ilivyoainishwa katika Sheria;

"MARPOL" maana yake ni Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi Utokanao na Meli, 1973 kama ulivyorekebishwa;

"meli" maana yake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria;

"meli ya abiria" maana yake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria;

"meli iliyokuwepo" maana yake ni meli ambayo si meli mpya;

"meli mpya" maana yake ni meli ambayo-

(a) mkuku wake ulilazwa; au

(b) kwa kiasi kikubwa-

(i) imefanyiwa mabadiliko; au

(ii) imejengwa upya;

"Meli ya Tanzania" maana yake ni meli iliyosajiliwa au kupewa leseni chini ya masharti ya Sheria kwenye bandari iliyo katika Jamhuri ya Muungano;

"MEPC" maana yake ni Kamati ya Ulinzi wa Mazingira ya Baharini ya IMO;

Sura ya 165 "mkaguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kama mkaguzi chini ya kifungu cha 382(1) cha Sheria;

"Mkataba" maana yake ni Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi kutoka Melini wa Mwaka 1973 kama ulivyorekebishwa;

Sura ya 166 "Mkuu wa Bandari" maana yake ni Mkuu wa Bandari aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 36 cha Sheria ya Bandari;

"mmiliki au mmiliki wa meli" maana yake, kuhusiana na meli iliyosajiliwa, mmiliki aliyesajiliwa na inajumuisha mkodishwaji na mmiliki mwendeshaji au wakala mwendeshaji;

Sura ya 415 "Msajili" maana yake ni Msajili aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania;

"nchi inayopeperusha bendera" kuhusiana na meli maana yake ni nchi ambayo meli ina haki ya kupeperusha bendera yake;

"Safari ya kimataifa" maana yake ni safari ya baharini kutoka bandarini au mahali popote katika Jamhuri ya Muungano hadi bandarini au nje ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano, au kinyume chake;

Sura ya 165 "Sheria" maana yake ni Sheria ya Usafirishaji Majini;

Sura ya 415 "Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania;

"shirika linalotambulika" maana yake ni Shirika ambalo limefanyiwa tathmini na Shirika na kubainika kuwa linazingatia Kanuni za kimataifa za shirika linalotambulika;

"tangi la kutunzia" maana yake ni tangi linalotumika kukusanya na kuhifadhi majitaka;

"tarehe ya ukomo wa muda", kuhusiana na Cheti cha Majitaka ya meli, maana yake ni siku ya mwisho ya kipindi kilichoainishwa katika Cheti cha Majitaka kama kipindi ambacho Cheti hicho ni halali;

"ubadilishaji wa moja kwa moja" maana yake ni ubadilishaji wa moja kwa moja wa vifaa vinavyoendana na mahitaji husika yanayotumika kwenye meli hiyo;

"utiririshaji" kuhusiana na maji taka, maana yake ni utoaji wowote unaosababishwa kwa namna yoyote kutoka kwenye meli, na inajumuisha utokaji wowote, uondoshaji, umwagikaji, uvujaji, usukumaji, utoaji au umwagaji;

"UNCLOS" maana yake ni Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari ya Mwaka 1982; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya usafiri majini.

Rejea inayofanana

**4.**-(1) Rejea katika Mkataba, Kiambatisho cha Mkataba au Kanuni za Eneo la Ncha za Dunia katika Kanuni hizi itafasiriwa-

(a) kama rejea ya Mkataba, Kiambatisho cha Mkataba au Kanuni za Eneo la Ncha za Dunia kama inavyorekebishwa mara kwa mara; na

(b) iwapo Mkataba, Kiambatisho cha Mkataba au Kanuni ya Eneo la Ncha za Dunia zitabadilishwa, kama rejea ya mabadiliko hayo.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), Mkataba, Kiambatisho cha Mkataba au Kanuni za Eneo la Ncha za Dunia zinarekebishwa au kubadilishwa iwapo marekebisho au mabadiliko yataanza kutekelezwa kwa mujibu wa Ibara ya 16 ya Mkataba.

(3) Marekebisho au mabadiliko ya Mkataba, Kiambatisho cha Mkataba au Kanuni za Eneo la Ncha za Dunia yatatekelezwa wakati marekebisho au mabadiliko hayo yanapoanza kutumika kwa mujibu Ibara ya 16 ya Mkataba.

## SEHEMU YA PILI
## UTIRIRISHAJI MAJI TAKA

Katazo la kutiririsha maji taka

**5**.-(1) Mmiliki wa meli au nahodha hataruhusiwa kutiririsha majitaka kutoka kwenye meli ambayo si meli ya abiria isipokuwa kama-

(a) meli inatiririsha majitaka-

(i) yaliyotibiwa kwa kutumia mfumo ulioidhinishwa na Shirika kwa mujibu wa kanuni ya 6, kwa umbali wa zaidi ya maili 3 kutoka ardhi iliyo karibu;

(ii) ambayo hayajatibiwa kwa umbali wa zaidi ya maili 12 kutoka ardhi iliyo karibu;

(iii) ambayo yamehifadhiwa kwenye tangi la kuhifadhia majitaka, au majitaka kutoka sehemu ya kuhifadhia wanyama kwa kiwango cha wastani wakati meli inatembea kwa mwendo usiopungua noti 4:

Isipokuwa kwamba, kiwango cha umwagaji kinachorejewa chini ya aya ya (a) (ii) na (iii) kitaidhinishwa na Shirika kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa chini ya Jedwali la Kwanza; au

(b) umwagaji unaorejewa katika aya ya (a) unatekelezwa na meli ambayo inaendesha mtambo wa kusafisha majitaka ulioidhinishwa na kuthibitishwa na Shirika kukidhi mahitaji ya uendeshaji yaliyorejewa katika kanuni ya 6(1)(a), na majitaka hayatazalisha yabisi inayoonekana inayoelea wala kusababisha kubadilika rangi kwa maji yanayozunguka.

(2) Masharti ya kanuni ndogo ya (1) hayatatumika kwa meli inayofanya kazi katika maji ya Tanzania na meli zinazoingia nchini kutoka mataifa mengine zikiwa ndani ya maji ya Tanzania na zinatiririsha majitaka kwa masharti nafuu yatakayowekwa na Jamhuri ya Muungano.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (4), utiririshaji wa maji taka kutoka kwenye meli ya abiria ndani ya eneo maalumu umezuiliwa isipokuwa kama-

(a) meli inatumia mitambo ya kutibu maji taka iliyoidhinishwa na Utawala kukidhi vigezo vya uendeshaji vilivyorejewa katika kanuni ya 6(1)(a); na

(b) majitaka hayazalishi yabisi inayoonekana inaelea au kusababisha kubadilika rangi kwa maji yanayozunguka.

(4) Endapo majitaka yanayorejewa chini ya Kanuni hizi yamechanganywa na taka au majitaka yenye masharti tofauti ya utiririshaji chini ya kanuni nyingine zilizotengenezwa chini ya Sheria, masharti magumu zaidi ya utiririshaji yatatumika.

(5) Masharti ya kanuni hii hayatatumika iwapo-

(a) umwagaji majitaka ni lazima kwa madhumuni ya-

(i) kulinda usalama wa meli na watu waliomo ndani ya meli; au

(ii) kuokoa maisha baharini;

(b) umwagaji wa majitaka-

(i) unatokana na uharibifu wa meli au vifaa vyake; na

(ii) pale ambapo tahadhari zote zinazofaa zimechukuliwa kabla na baada kutokea uharibifu ili kuzuia au kupunguza utiririshaji.

## SEHEMU YA TATU
## VIFAA NA UDHIBITI WA UTIRIRISHAJI

Mifumo ya majitaka

**6**.-(1) Meli ambayo, kwa mujibu wa kanuni ya 2(2), inatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi itawekewa mojawapo ya mifumo ya majitaka ifuatayo:

(a) mtambo wa kusafisha majitaka wa aina iliyoidhinishwa na Shirika, kwa kuzingatia viwango na mbinu za majaribio zilizotengenezwa na IMO kwa mapendekezo ya viwango vya kimataifa vya uchafu na miongozo ya vipimo vya utendaji wa mitambo ya kutibu majitaka kwa mujibu wa azimio la MEPC.2(VI); au

(b) mfumo wa kupitisha majitaka na kuua viini ulioidhinishwa na Shirika na kuwekwa vifaa kwa ajili ya uhifadhi wa muda wa majitaka wakati meli ikiwa umbali wa chini ya maili 3 kutoka ardhi iliyo karibu.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), meli ya abiria ambayo inatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, na ambayo kanuni ya 5(3) inatumika ikiwa katika eneo maalumu, itawekewa mojawapo ya mifumo ya majitaka ifuatayo:

(a) mtambo wa kusafisha majitaka wa aina iliyoidhinishwa na Shirika, kwa kuzingatia viwango na vipimo kwa mujibu wa azimio la MEPC.2(VI); au

(b) tangi la kuhifadhia lenye uwezo ulioidhinishwa na Shirika kwa ajili ya kuhifadhi majitaka yote, kwa kuzingatia uendeshaji wa meli, idadi ya watu waliomo ndani na masuala mengine muhimu.

(3) Tangi la kuhifadhia lenye uwezo wa kuhifadhi majitaka, kwa kuzingatia uendeshaji wa meli, idadi ya watu waliomo ndani na mambo mengine muhimu yaliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1)(b) na (2)(b) litajengwa na kuwa na namna ya kuonesha kiasi cha taka zilizomo.

Viunganishi vya utiririshaji

**7.**-(1) Bomba la kutiririsha majitaka la meli litafungwa viunganishi vya kawaida vya kutiririsha maji taka ili kuliwezesha kuunganishwa kwenye bomba la miundombinu ya kupokelea majitaka kwa mujibu wa vipimo mahususi kwa ajili ya viunganishi vya kutiririsha maji taka kama ilivyoainishwa chini ya Jedwali la Pili.

(2) Kwa meli inayofanya biashara maalumu ya abiria, bomba la meli la kutiririsha inaweza kufungwa na kiunganishi cha kumwaga majitaka kinachokubaliwa na Shirika, kama kiunganishi cha haraka.

## SEHEMU YA NNE
## UKAGUZI NA UTHIBITISHAJI WA MELI

Ukaguzi

**8.**-(1) Meli ambayo inatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi itatakiwa kufanyiwa ukaguzi ufuatao:

(a) ukaguzi wa awali kabla ya meli kuanza kutumika au kabla Cheti kinachohitajika chini ya kanuni ya 9 hakijatolewa kwa mara ya kwanza, ambao utajumuisha ukaguzi kamili wa muundo, vifaa, mifumo, viunganishi, mipangilio na nyenzo kwa kadiri meli inavyosimamiwa na Kanuni hizi;

(b) ukaguzi wa uhuishaji kwa vipindi vilivyoainishwa na Shirika, visivyozidi miaka mitano, isipokuwa pale ambapo kanuni ya 13 (2), (3), (4), (5), (6), (7) na (8) zinatumika:

Isipokuwa kwamba, ukaguzi unaorejewa chini ya aya ya (a) na (b) utahakikisha kwamba muundo, vifaa, mifumo, viunganishi, mipangilio na nyenzo unakidhi kikamilifu masharti husika ya Kanuni hizi;

(c) ukaguzi wa ziada, wa jumla au wa sehemu, kulingana na mazingira, utafanywa baada ya matengenezo yanayotokana na uchunguzi ulioainishwa chini ya kanuni ndogo ya (4), au wakati wowote ambapo matengenezo au uhuishaji unapofanyika:

Isipokuwa kwamba, ukaguzi unaorejewa chini ya aya (c) utahakikisha kwamba matengenezo au uhuishaji muhimu umefanyika ipasavyo na kwamba nyenzo na utaalamu wa matengenezo au uhuishaji huo unaridhisha na kwamba meli inakidhi masharti ya Kanuni hizi;

TS Na. 106 la 2006

(2) Meli ambayo haiko chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1) itazingatia masharti ya Kanuni za Meli Ndogo, Usalama wa Meli za Mizigo za Ndani, Usalama wa Meli Ndogo, Ukaguzi na Uchunguzi wa Meli Zinazofanya Biashara na Safari za Ndani na Maji ya Ndani ya Nchi.

(3) Mkaguzi anaweza-

(a) kuhitaji kufanyika kwa matengenezo ya meli; na

(b) kufanya ukaguzi iwapo ataombwa na mamlaka husika kwenye bandari meli ilipofikia.

(4) Pale ambapo mkaguzi atabaini kwamba-

(a) kwa kiasi kikubwa hali ya meli au vifaa vyake havishabihiani na taarifa za kwenye Cheti cha Majitaka; au

(b) meli haifai kuingia baharini bila kuonesha viashiria hatarishi vya kusababisha athari kwa mazingira ya majini,

Mkaguzi huyo atahakikisha kwamba hatua za kurekebisha zinachukuliwa mara moja na kulitaarifu Shirika kwa wakati.

(5) Endapo hatua za kurekebisha zinazorejewa chini ya kanuni ndogo ya (5) hazijachukuliwa, Cheti cha Majitaka kitasimamishwa na Shirika na iwapo meli ipo kwenye bandari ya nchi mwanachama wa Mkataba, Cheti cha Majitaka kitasimamishwa na mamlaka husika ya bandari meli ilipofikia.

(6) Endapo Shirika au shirika linalotambulika au mamlaka ya uthibitishaji itasimamisha uhalali wa Cheti cha Majitaka kilichotolewa kwa meli, itatoa mara moja notisi ya maandishi ya kusimamishwa huko-

(a) kwa mmiliki wa meli; na

(b) iwapo meli ipo kwenye bandari iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano, kwa mamlaka zinazohusika na usafiri wa majini za

nchi ambayo bandari hiyo ipo.

(7) Endapo afisa au mkaguzi wa nchi mwanachama wa Mkataba, amelitaarifu Shirika kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (6), Shirika litampatia afisa au mkaguzi huyo usaidizi wowote muhimu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao chini ya kanuni hii.

(8) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (7), Shirika litahakikisha pale inapowezekana kwamba meli haianzi safari hadi pale ambapo inaweza kuingia baharini au kuondoka bandarini kwa madhumuni ya kuingia sehemu ya karibu ya matengenezo bila kusababisha madhara kwenye mazingira ya majini.

(9) Shirika litahakikisha kwamba-

(a) hali ya meli na vifaa vyake inaimarishwa ili kuendana na masharti ya Kanuni hizi; na

(b) meli kwa namna yoyote inabakia kuwa sawa na kuingia baharini bila kuonesha tishio la kusababisha athari kwa mazingiza ya majini.

(10) Baada ya kukamilika kwa uchunguzi wowote wa meli chini ya kanuni ndogo ya (1), mabadiliko hayatafanyika katika muundo, vifaa, mifumo, viunganishi, mipangilio au nyenzo zilizokaguliwa ,bila idhini ya Shirika, isipokuwa ubadilishaji wa moja kwa moja wa vifaa na viunganishi hivyo.

(11) Endapo ajali inatokea kwenye meli au hitilafu itagundulika ambayo kwa kiasi kikubwa inaathiri utendaji wa meli au ufanisi au ukamilifu wa vifaa vyake vilivyoainishwa na Kanuni hizi, nahodha au mmiliki wa meli atatoa taarifa mapema kwa Shirika au shirika linalotambulika lenye jukumu la kutoa Cheti husika, ambalo litaelekeza uchunguzi kuanzishwa ili kubaini endapo ukaguzi chini ya kanuni ndogo ya (1), ya kanuni hii unahitajika.

(12) Endapo meli inayorejewa chini ya kanuni ndogo ya (11), ipo katika bandari ya nchi nyingine mwanachama wa Mkataba, nahodha au mmiliki atatoa taarifa mara moja kwa mamlaka husika ya nchi ambapo meli imefikia na Shirika au shirika linalotambulika litahakikisha kwamba taarifa hiyo imetolewa.

(13) Endapo kuna mgogoro wa kuhusiana matengenezo au uhuishaji uliofanyika au unaotegemea kufanyika katika meli ni matengenezo au uhuishaji muhimu kwa madhumuni ya kanuni hii, mmiliki au nahodha wa meli anaweza kuwasilisha ombi kwa maandishi kwa Shirika kuomba ushauri.

(14) Matengenezo au uhuishaji hautachukuliwa kuwa muhimu kwa madhumuni ya kanuni hii isipokuwa kama Shirika linashauri vinginevyo ndani ya siku ishirini na moja baada ya kupokea ombi chini ya kanuni ndogo ya (13).

Utoaji au uidhinishaji wa Cheti

**9**.-(1) Cheti cha Majitaka kitatolewa, baada ya uchunguzi wa awali au uhuishaji kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 8, kwa meli yoyote ambayo inafanya safari kwenda kwenye bandari au vituo vya baharini vilivyopo chini ya mamlaka ya nchi nyingine wanachama wa Mkataba.

(2) Cheti kilichorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitatolewa na Shirika au shirika linalotambulika au lilioidhinishwa na Shirika na Shirika au shirika linalotambulika litawajibika kikamilifu kuhusiana na Cheti hicho.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2) Cheti kilichotolewa na shirika linalotambulika kitakuwa na maelezo kwamba kimetolewa kwa ombi la Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kitakuwa na nguvu sawa na kutambuliwa sawa na Cheti kilichotolewa na Shirika.

(4) Cheti cha Majitaka hakitatolewa kwa meli ambayo inapeperusha bendera ya nchi ambayo siyo Mwanachama wa Mkataba.

Utoaji au uudhinishaji wa Cheti na nchi nyingine Mwanachama

**10.**-(1) Shirika linaweza kuuomba nchi mwanachama wa Mkataba kukagua meli ya Tanzania na, ikiwa nchi hiyo imeridhika kwamba meli inakidhi matakwa ya Kiambatisho cha IV cha Mkataba, itatoa au kuidhinisha kuolewa Cheti cha Majitaka kwa meli hiyo na pale inapobidi kuidhinisha au kuridhia kuidhinishwa kwa Cheti hicho kwenye meli kwa mujibu wa Kiambatisho hicho.

(2) Endapo Cheti cha Majitaka kimetolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1)-

(a) Shirika litachukuliwa kama mamlaka ya uthibitishaji kuhusiana na Cheti hicho; na

(b) rejea yoyote ya mamlaka ya uthibitishaji iliyotoa Cheti katika Kanuni hizi itachukuliwa kama rejea ya Shirika.

Utoaji au uidhinishaji wa Cheti cha serikali nyingine

**11**.-(1) Shirika linaweza, kwa ombi la mamlaka ya serikali nyingine mwanachama wa Mkataba, kuhakikisha meli inakaguliwa na ikiwa litaridhika kwamba masharti ya Kanuni hizi na Kiambatisho cha IV cha Mkataba yamezingatiwa, litatoa au kuidhinisha utoaji wa Cheti cha Majitaka kwa meli hiyo.

(2) Nakala ya Cheti na nakala ya taarifa ya ukaguzi zitatumwa kwa mamlaka ya nchi iliyoomba uchunguzi.

(3) Cheti kinachorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitakuwa na taarifa kwamba kimetolewa kwa ombi la mamlaka ya nchi hiyo na kitakuwa na nguvu na kutambulika sawa na Cheti kilichotolewa chini ya kanuni ya 9.

Muundo wa Cheti

**12.**-(1) Cheti cha Majitaka kitakuwa kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Cheti cha Msahama cha Kuzuia Utiririshaji Majitaka Baharini kwa Mashua zisizojiendesha zenyewe na zisizokuwa na nahodha au wafanyakazi kitakuwa kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Nne.

Muda na uhalali wa Cheti

**13**.-(1) Cheti cha Majitaka kitatolewa kwa muda wa miaka mitano kuanzia tarehe ya kutolewa.

(2) Bila kujali matakwa ya kanuni ndogo ya (1), ukaguzi wa kuhuisha ukikamilika-

(a) ndani ya miezi mitatu kabla ya tarehe ya ukomo wa Cheti kilichopo, Cheti kipya kitakuwa halali kuanzia tarehe ya kukamilika kwa ukaguzi wa kuhuisha hadi tarehe isiyozidi miaka mitano kuanzia tarehe ya ukomo wa Cheti kilichopo;

(b) baada ya tarehe ya ukomo wa Cheti kilichopo, Cheti kipya kitakuwa halali kuanzia tarehe ya kukamilika kwa ukaguzi wa kuhuisha hadi tarehe isiyozidi miaka mitano kuanzia tarehe ya ukomo wa kuhuisha Cheti kilichopo;

(c) zaidi ya miezi mitatu kabla ya tarehe ya ukomo wa Cheti kilichopo, Cheti kipya kitakuwa halali kuanzia tarehe ya kukamilika kwa ukaguzi wa kuhuisha hadi tarehe isiyozidi miaka mitano kuanzia tarehe ya kukamilika kwa ukaguzi wa kuhuisha.

(3) Endapo Cheti kimetolewa kwa muda usiozidi miaka mitano, Shirika linaweza kuongeza muda wa uhalali wa Cheti zaidi ya tarehe ya ukomo wa matumizi hadi muda wa juu uliotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1).

(4) Endapo ukaguzi wa kuhuisha umekamilika na Cheti kipya hakiwezi kutolewa au kuwekwa melini kabla ya tarehe ya kuisha kwa Cheti kilichopo, Shirika linaweza kuidhinisha Cheti kilichopo na Cheti hicho kitakubalika kama Cheti halali kwa kipindi kingine kisichozidi miezi mitano kutoka tarehe ya ukomo.

(5) Endapo meli wakati Cheti kinaisha muda wake haipo katika bandari au kituo cha baharini ambapo itakaguliwa, Shirika linaweza kuongeza muda wa uhalali wa Cheti isipokuwa nyongeza hii itatolewa kwa madhumuni ya kuruhusu meli kukamilisha safari yake ya kuelekea bandarini ambapo itakaguliwa na katika mazingira ambayo itaonekana inafaa na ni muhimu kufanya hivyo.

(6) Cheti hakitaongezewa muda zaidi ya miezi mitatu, na meli inayoongezewa muda huo, wakati wa kuwasili katika bandari ambayo itakaguliwa, haitaruhusiwa kwa mujibu wa nyongeza hiyo kuondoka kwenye bandari hiyo bila kuwa na Cheti kipya na pale ambapo ukaguzi wa kuhuisha umekamilika, Cheti kipya kitakuwa halali hadi tarehe isiyozidi miaka mitano kuanzia tarehe ya ukomo wa Cheti kilichopo kabla ya kutolewa kwa nyongeza.

(7) Cheti kinachotolewa kwa meli inayojihusisha na safari fupi ambayo haijaongezewa muda chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (5) na (6) inaweza kuongezewa muda na Shirika kwa muda wa ziada hadi mwezi mmoja kutoka tarehe ya ukomo ulioanishwa kwenye Cheti hicho na pale ambapo ukaguzi wa kuhuisha umekamilika Cheti kitakua halali hadi tarehe isiyozidi miaka mitano kutoka tarehe ya ukomo wa Cheti kilichopo kabla ya kutolewa kwa nyongeza ya muda.

(8) Katika mazingira maalumu na kama itakavyoamuliwa na Shirika, Cheti kipya kinaweza kisipewe tarehe kutoka tarehe ya ukomo wa Cheti kilichopo kama inavyotakiwa chini ya kanuni ndogo ya (2)(b), (5) au (7) na Cheti hicho kipya kitakuwa halali hadi tarehe isiyozidi miaka mitano kutoka tarehe ya kukamilika kwa ukaguzi wa kuhuisha.

(9) Cheti kilichotolewa chini ya kanuni hii kitakoma kuwa halali kwa mazingira yafuatayo:

(a) pale ambapo mabadiliko makubwa yamefanyika katika vifaa, viunganishi, mpangilio au nyenzo za meli zinazohitajika bila idhini ya Shirika, isipokuwa ubadilishaji wa moja kwa moja wa vifaa au viunganishi hivyo;

(b) pale ambapo ukaguzi husika haujakamilika ndani ya muda ulioainishwa chini ya kanuni ya 8(1); au

(c) baada ya kuhamishwa kwa meli kwenye bendera ya nchi nyingine.

(10) Shirika litatoa Cheti kipya kwa meli iliyohamishwa pale litakaporidhika kwamba meli hiyo inazingatia matakwa ya kanuni ya 8(9) na (10).

(11) Ikiwa ni uhamisho wa meli ya Tanzania kwenda nchi mwanachama wa Mkataba, iwapo itaombwa ndani ya miezi mitatu baada ya uhamisho kufanyika, Shirika ndani ya mwezi mmoja, litapeleka kwa mamlaka ya nchi nyingine nakala za vyeti vya meli inayohamishwa na nakala za taarifa za ukaguzi husika ikiwa zinapatikana.

(12) Baada ya kuhamishwa kwa meli ya Tanzania, Cheti cha meli iliyohamishwa kitaendelea kutumika kwa muda usiozidi miezi mitano isipokuwa kwamba muda wake hautakoma kabla ya mwisho wa kipindi hicho, au hadi Shirika litoe Cheti mbadala.

(13) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (9)(c), Shirika litaomba

nakala ya Cheti kilichobebwa na meli kabla ya uhamisho kufanyika kutoka kwa serikali ya nchi wanachama ambayo awali meli ilikuwa na haki yakupeperusha bendera yake na nakala ya taarifa ya ukaguzi husika inapatikana.

Katazo kwa meli ya Tanzania kufanya safari bila Cheti cha Majitaka

**14**. Kwa kuzingatia kanuni ya 21(2), meli ya Tanzania ambayo Kanuni hizi zinatumika-

(a) haitaenda baharini; au

(b) ikiwa tayari iko baharini, haitabaki baharini:

Isipokuwa kama-

(i) ukaguzi wa awali au ukaguzi wa kuhuisha umefanyika katika meli hiyo; na

(ii) Cheti cha Majitaka kimetolewa kwa meli hiyo na bado ni halali.

Katazo kwa meli isiyo ya Tanzania kuingia baharini

**15.** Meli ya nchi wanachama wa Mkataba haitaingia baharini kutoka bandari ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa kama-

(a) Cheti cha Majitaka kimetolewa kwa mujibu wa Kiambatisho cha IV kuhusiana meli hiyo na bado ni halali;

(b) mkaguzi ameridhika kwamba meli inaweza kufanya safari baharini bila kuonesha viashiria hatarishi vya kusababisha athari kwenye mazingira ya bahari; au

(c) mtu mwenye mamlaka ya kushikilia meli ameiruhusu meli hiyo kuingia baharini kwa madhumuni ya kwenda kwenye karakana ya karibu ya ukarabati inayopatikana eneo la karibu.

Majukumu ya mmiliki na nahodha wa meli ya Tanzania

**16**. Mmiliki na nahodha wa meli ya Tanzania atahakikisha kwamba-

(a) hali ya meli na vifaa vyake inaimarishwa na kwa namna yoyote inaendelea na safari bila kuonesha viashiria hatarishi vya kusababisha athari kwa mazingira majini;

(b) baada ya ukaguzi wowote wa meli unaohitajika na Sehemu hii kukamilika, hakuna mabadiliko isipokuwa kwa njia ya ubadilishaji wa moja kwa moja, yatakayofanywa kwa muundo, vifaa, mifumo, viunganishi, mipangilio au nyenzo za meli hiyo, bila idhini ya Shirika;

(c) endapo ajali imetokea kwa meli ya Tanzania au hitilafu imegundulika kwa meli ya Tanzania ambayo kwa kiwango kikubwa inaathiri ubora, ufanisi au utimilifu wa vifaa vya meli kama inavyotakiwa chini ya Sehemu ya Tatu:

(i) taarifa kuhusu ajali au hitilafu itatolewa mapema iwezekanavyo kwa Shirika au shirika linalotambulika lililotoa Cheti cha Majitaka kuhusiana na meli hiyo; na

(ii) kwa meli iliyopo katika bandari nje ya Jamhuri ya Muungano, taarifa kuhusu ajali au hitilafu hiyo itatolewa kwa mamlaka iliyopo katika nchi ambayo bandari hiyo ipo.

Masharti mengineyo kuhusiana na Cheti cha Majitaka

**17.**-(1) Shirika linaweza kufuta Cheti cha Majitaka kilichotolewa kwa meli ya Tanzania iwapo kuna sababu ya kuamini kwamba-

(a) Cheti cha Majitaka kilitolewa kwa taarifa za uongo au zenye makosa; au

(b) tangu kukamilika kwa ukaguzi wowote unaohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi, muundo, vifaa, mifumo, viunganishi, mipangilio na nyenzo za meli zimepata uharibifu au zina upungufu.

(2) Shirika linaweza kuhitaji kurudishwa kwa Cheti cha Majitaka kilichotolewa kwa meli ya Tanzania iwapo Cheti hicho kimefikia ukomo, kimesimamishwa au kimefutwa.

(3) Maelekezo yaliyotolewa na Shirika chini ya kanuni ndogo ya (2) yanaweza kubainisha kwamba Cheti cha Majitaka kitarudishwa ndani ya muda na kwa namna ambayo Shirika linaweza kuelekeza.

(4) Kwa meli za Tanzania, mtu hatapaswa-

(a) kubadili kwa makusudi Cheti cha Majitaka, isipokuwa kama ameruhusiwa kufanya hivyo chini ya Kanuni hizi;

(b) kwa makusudi kutengeneza Cheti cha Majitaka cha kughushi;

(c) kwa kujua au kwa uzembe kutoa taarifa za uongo kuhusiana na ukaguzi unaohitajika chini ya Kanuni hizi;

(d) kwa nia ya kudanganya, kutumia au kukopesha Cheti cha Majitaka au kuruhusu Cheti cha Majitaka kutumiwa na mtu mwingine; au

(e) kukataa kurudisha Cheti cha Majitaka pale anapohitajika kufanya hivyo chini ya kanuni ndogo ya (2).

(5) Mmiliki na nahodha wa meli, ambaye amepewa Cheti cha Majitaka, atahakikisha kwamba Cheti hicho kinapatikana kwa urahisi ndani ya meli muda wote, isipokuwa pale ambapo kimerejeshwa chini ya kanuni ndogo (2).

(6) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kanuni ndogo za (4) na (5) anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote.

## SEHEMU YA TANO
## UTEKELEZAJI

Ukaguzi wa meli

**18.**-(1) Mamlaka ya kukagua meli na vifaa vyake, sehemu yoyote ya meli, kifaa chochote ndani ya meli na nyaraka yoyote inayobebwa ndani ya

meli, yatakomea kwenye-

(a) kuthibitisha kama majitaka yametiririshwa kutoka melini kinyume na Kanuni hizi;

(b) kuchunguza shughuli yoyote inayodhibitiwa na Kanuni hizi, endapo kuna sababu ya wazi ya kuamini kwamba nahodha au mfanyakazi wa melini hana uelewa wa taratibu muhimu za meli zinazohusiana na kuzuia uchafuzi unaotokana na majitaka;

(c) kuthibitisha endapo Cheti cha Majitaka kimetolewa kuhusiana na meli na bado ni halali; au

(d) kuthibitisha endapo nyaraka sahihi zimetolewa kuhusiana na meli na bado ni halali.

(2) Mamlaka ya kupanda melini kufanya ukaguzi yanaweza kutumika pale ambapo meli-

(a) ipo katika bandari ya Jamhuri ya Muungano;

(b) ipo kwenye kituo cha baharini katika maji ya Tanzania au maji yaliyodhibitiwa;

(c) ni chombo cha kudumu kilichosimikwa katika maji ya Tanzania au maji yaliyodhibitiwa; au

(d) ni chombo kinachoelea katika maji ya Tanzania au maji yaliyodhibitiwa, tofauti na chombo kinachoelea ambacho kinapita.

(3) Endapo meli inakaguliwa kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1)(a) na si meli ya Tanzania, mtu anayetekeleza mamlaka ya ukaguzi atahakikisha kwamba taarifa ya ukaguzi inatumwa kwa-

(a) mwakilishi wa kidiplomasia wa nchi inayopeperusha bendera ya meli au mamlaka husika za usafiri majini za nchi hiyo; na

(b) nchi nyingine yoyote mwanachama wa Mkataba ambayo iliomba ukaguzi.

Masharti ya kushikilia meli

**19.**-(1) Endapo mkaguzi wa meli ana sababu kuamini kwamba-

(a) Cheti cha Majitaka kilitakiwa kuwa kimetolewa kuhusiana na meli lakini hakijatolewa, au kilitolewa lakini si halali;

(b) nyaraka sahihi ilitakiwa kuwa imetolewa kuhusiana na meli lakini haijatolewa, au imetolewa lakini si halali;

(c) hali ya meli au vifaa vyake havilandani kwa kiasi kikubwa na taarifa zilizopo kwenye Cheti hicho au nyaraka nyingine inayotakiwa;

(d) nahodha au mfanyakazi wa meli hana uelewa wa taratibu muhimu za melini zinazohusiana na kuzuia uchafuzi unaotokana wa maji taka; au

(e) kosa chini ya kanuni ya 22(2) (d) limefanywa kuhusiana na meli,

meli iitazuiliwa hadi mkaguzi wa meli atakaporidhika kwamba inaweza kuelekea baharini bila kuonesha viashiria hatarishi vya kusababisha athari kwa mazingira bahari.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtu mwenye mamlaka ya kuzuia meli anaweza kuruhusu meli inayotakiwa kuzuiliwa chini ya kanuni ndogo ya (1) kuingia baharini kwa madhumuni ya kwenda kwenye karakana sahihi ya karibu zaidi inayopatikana.

(3) Mamlaka ya kuzuia meli chini ya Kanuni hii inaweza kutumika endapo meli-

(a) ipo katika bandari ya Jamhuri ya Muungano;

(b) ipo kwenye kituo cha baharini katika maji ya Tanzania au maji yaliyodhibitiwa;

(c) ni chombo cha kudumu kilichosimikwa katika maji ya Tanzania au maji yaliyodhibitiwa; au

(d) ni chombo kinachoelea katika maji ya Tanzania au maji yaliyodhibitiwa, tofauti na chombo kinachoelea ambacho kinapita.

(4) Masharti ya kifungu cha 409 cha Sheria, isipokuwa kifungu kidogo cha (7), yatatumika pale ambapo meli inapaswa kuzuiwa chini ya masharti yaliyotangulia ya kanuni hii kana kwamba rejea za uzuiaji wa meli chini ya Sheria zilikuwa ni rejea za uzuiaji wa meli husika chini ya masharti yaliyotangulia ya kanuni hii.

(5) Endapo ambapo meli inapaswa kuzuiwa chini ya kanuni hii, mtu anayeizuia meli hiyo atampatia nahodha wa meli hiyo notisi ya zuio ambayo-

(a) itaeleza sababu za kuzuia; na

(b) itahitaji masharti ya notisi yazingatiwe hadi meli itakapoachiwa na mtu yeyote aliyetajwa katika kifungu cha 383(1) cha Sheria.

(6) Endapo meli nyingine isiyo ya Tanzania imezuiliwa, Shirika litamtaalifu mwakilishi wa kidiplomasia wa nchi inayopeperusha bendera ya meli au mamlaka husika za usafiri majini za nchi hiyo.

(7) Endapo meli imezuiwa chini ya kanuni ndogo ya (3), mtu mwenye mamlaka ya kuizuia meli atapaswa, kwa ombi la mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha, kuachia meli hiyo-

(a) ikiwa hakuna shauri la kosa chini ya kanuni ya 24(1)(d) lililofunguliwa ndani ya muda wa siku saba kuanzia siku ambayo meli imezuiwa;

(b) ikiwa shauri la kosa chini ya kanuni ya 22(2)(d), baada ya kuwa limefunguliwa ndani ya muda huo, limetolewa maamuzi bila mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha kutiwa hatiani;

(c) ikiwa-

(i) jumla ya shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu moja na mia tano zinalipwa kwa Waziri kwa njia ya dhamana; au

(ii) dhamana ambayo, kwa maoni ya Waziri, inajitosheleza na ni kwa kiasi kisichopungua shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu hamsini inatolewa kwa Waziri au kwa niaba ya nahodha au mmiliki,

na au kwa niaba ya mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha;

(d) Baada ya mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha kutiwa hatiani kwa kosa lolote kama hilo, ikiwa gharama au matumizi yoyote yameamuliwa kulipwa na mtu huyo, na faini yoyote iliamriwa kulipwa na mtu huyo imelipwa; au

(e) amri ya kuachiwa imetolewa na mahakama au baraza liliorejewa chini ya Ibara ya 292 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari ya 1982 na dhamana yoyote au dhamana ya kifedha nyingine iliyoamriwa na mahakama au baraza hilo imetolewa.

(8) Waziri atarejesha kiasi chochote kilicholipwa kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (7)(c) au kuondoa dhamana yoyote iliyowekwa iwapo-

(a) hakuna shauri la kosa chini ya kanuni ya 22(2)(d) lililofunguliwa ndani ya muda wa siku saba kuanzia siku ambayo kiasi hicho kililipwa; au

(b) mwenendo wa shauri la kosa hilo, baada ya kuwa limefunguliwa ndani ya muda huo, maamuzi yametolewa bila ya mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha kutiwa hatiani.

(9) Endapo jumla imelipwa, au dhamana imetolewa, na mtu yeyote kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (7)(c) na mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha ametiwa hatiani kwa kosa chini ya kanuni ya 22(2)(d), kiasi kilicholipwa au kiasi kilitolewa chini ya dhamana kitatumika kama ifuatavyo-

(a) kwanza, kwa kulipa gharama au matumizi yaliyoamriwa na mahakama kulipwa na nahodha au mmiliki; na

(b) malipo yanayofata ya faini yoyote iliyotolewa na mahakama,

na kiasi kilichobaki kitalipwa na mtu anayelipa, au kutoa dhamana.

Mamlaka ya Mkuu wa Bandari kushikilia meli

**20**.-(1) Endapo Mkuu wa Bandari iliyopo Jamhuri ya Muungano ana sababu za wazi za kuamini kwamba kosa limefanyika chini ya kanuni ya 22(2)(d) kwa kutiririsha majitaka kwenye maji ya bandari, Mkuu wa Bandari anaweza kuzuia meli.

Sura. 166

(2) Masharti ya kifungu cha 55(4) cha Sheria ya Bandari yatatumika kwa zuio chini ya kanuni ndogo ya (1) kama yanavyotumika kwa zuio la kibali cha bandari.

(3) Endapo meli inatakiwa kuzuiwa chini ya kanuni hii, Mkuu wa Bandari anayeizuia meli atatakiwa kuwasilisha kwa nahodha wa meli notisi ya zuio ambayo-

(a) inaeleza sababu za zuio; na

(b) inahitaji masharti ya notisi kuzingatiwa hadi meli itakapoachiwa na Mkuu wa Bandari.

(4) Endapo meli imezuiwa chini ya kanuni hii, Mkuu wa Bandari atatakiwa, kwa ombi, kuachia meli hiyo-

(a) ikiwa hakuna shauri la kosa chini ya kanuni ya 22(2)(d) lililofunguliwa ndani ya muda wa siku saba kuanzia siku ambayo meli imezuiwa;

(b) ikiwa shauri la kosa chini ya kanuni ya 22(2)(d), baada ya kuwa limefunguliwa ndani ya muda huo, limetolewa maamuzi bila mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha kutiwa hatiani;

(c) ikiwa-

(i) jumla ya shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu moja na mia tano zinalipwa kwa Waziri kwa njia ya dhamana; au

(ii) dhamana ambayo, kwa maoni ya Waziri, inajitosheleza na ni kwa kiasi kisichopungua shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu hamsini inatolewa kwa Waziri au kwa niaba ya nahodha au mmiliki,

na au kwa niaba ya mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha;

(d) nahodha au mmiliki ametiwa hatiani kwa kosa, gharama na matumizi zilizoamriwa zitalipwa na yeye, na faini yoyote anayotakiwa kutoa, imelipwa; au

(e) kuachiwa kumeamriwa na mahakama au chombo cha kutoa haki kinachorejewa kwenye Ibara ya 292 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari, 1982, na dhamana au dhamana nyingine ya fedha aliyoamriwa na mahakama au chombo cha kutoa haki hicho imewekwa.

(5) Waziri atarejesha kiasi chochote kilicholipwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (4)(c) au kuachia dhamana yoyote iliyowekwa iwapo-

(a) hakuna shauri la kosa chini ya kanuni ya 22(2)(d) lililofunguliwa ndani ya muda wa siku saba kuanzia siku ambayo kiasi hicho kililipwa; au

(b) mwenendo wa shauri la kosa hilo, baada ya kuwa limefunguliwa ndani ya muda huo, maamuzi yametolewa bila ya mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha kutiwa hatiani.

(6) Endapo kiasi cha fedha kimelipwa, au dhamana imewekwa, na mtu yeyote kwamujibu wa kanuni ndogo ya (4) (c) na mmiliki, meneja, mkodishwaji au nahodha ametiwa hatiani kwa kosa chini ya kanuni ya 22(2)(d), kiasi kilicholipwa au kiasi kilitolewa chini ya dhamana kitatumika kama ifuatavyo-

(a) kwanza, kwa kulipa gharama au matumizi yaliyoamriwa na mahakama kulipwa na nahodha au mmiliki; na

(b) malipo yanayofata ya faini yoyote iliyotolewa na mahakama,

na kiasi kilichobaki kitalipwa na mtu anayelipa, au kutoa dhamana.

Wajibu wa Mkuu wa Bandari kutoa taarifa ya meli yenye upungufu

**21**. Mkuu wa Bandari wa bandari iliyopo Jamhuri ya Muungano atalitaarifu Shirika endapo Mkuu wa Bandari ana sababu za kuamini kwamba meli inakaribia kuingia bandarini; au kuondoka bandarini na haijazingatia masharti ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

**22**.-(1) Mmiliki wa meli na nahodha ambaye-

(a) anatiririsha maji taka kutoka kwenye meli kinyume na kanuni ya 5;

(b) anasababisha meli kuingia baharini bila-

(i) kuwa na Cheti kipya cha Majitaka kinyume na kanuni ya 13(6);

(ii) kufanya ukaguzi wa awali au ukaguzi wa kuhuisha kuhusiana na meli au bila kuwa na Cheti halali cha Majitaka kinyume na kanuni ya 14;

(iii) kibali cha mkaguzi au mtu mwenye mamlaka ya kuzuia meli na nyaraka kinyume na kanuni ya 15;

(iv) kuhakikisha kwamba hali ya meli na vifaa vyake vimeimarishwa ili kuendana na masharti ya Sehemu ya Tatu ya Kanuni hizi na inafaa kuingia baharini bila kuonesha viashiria hatarishi vya kusababisha athari kwa mazingira bahari kinyume na kanuni ya 16;

(v) kutoa taarifa ya ajali au hitilafu mapema iwezekanavyo kwa:

(aa) Shirika au shirika linalotambulika lililotoa Cheti cha Majitaka kuhusiana na meli ya Tanzania; au

(bb) mamlaka husika ya usafiri majini ikiwa meli ipo katika bandari iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano;

(vi) kuwa na taarifa ya ukaguzi inayoelezea uzingatiaji wa masharti chini ya Kanuni hizi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote.

(2) Mmiliki wa meli anayeshindwa kuzingatia masharti ya-

(a) kuwa na mtambo wa kutibu majitaka ulioidhinishwa na Shirika kinyume na kanuni ya 6(1)(a) na (2)(a);

(b) kuwa na mfumo wa kulainisha na kusafisha majitaka na kufungwa vifaa vilivyoidhinishwa na Shirika kinyume na kanuni ya 6(1)(b) na 2(a);

(c) kuwa na tangi la kuhifadhia lenye uwezo wa kuhifadhi majitaka yote linaloonyesha kwa macho kiasi cha kilichomo kinyume na kanuni ya 6(3);

(d) kuwa na bomba la kumwaga majitaka la meli lililofungwa kiunganishi cha kumwaga cha kawaida kinyume na kanuni ya 7,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote.

Adhabu ya jumla

**23**. Endapo mtu anatenda kosa ambalo hakuna adhabu maalumu iliyotolewa, endapo atatiwa hatiani chini ya Kanuni hizi, baada ya kutiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania sawa na dola za Marekani elfu moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA

Ushughulikiaji wa malalamiko
T.S Na. 338 la 2018

**24**. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa chini ya Kanuni hizi anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Shirika kwa mujibu wa Kanuni za Ushughulikiaji wa Malalamiko za Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania.

Tathmini na utoaji taarifa

**25**.-(1) Msajili-

(a) atafanya tathmini ya masharti ya udhibiti yaliyomo katika Kanuni hizi;

(b) ataandaa taarifa inayoainisha hitimisho la tathmini; na

(c) atawasilisha taarifa kwa Waziri.

(2) Taarifa ya kwanza itawasilishwa kwa Waziri ndani ya miaka mitano kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Kanuni hizi.

(3) Taarifa zinazofuata zitawasilishwa kwa vipindi visivyozidi miaka mitano.

(4) Taarifa chini ya kanuni hii-

(a) itaweka malengo yanayokusudiwa kufikiwa na kifungu cha udhibiti kinachorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1)(a);

(b) itatoa tathmini ya kiwango ambacho malengo hayo yatafikiwa; na

(c) itatathmini iwapo malengo hayo bado yanatija, na ikiwa ndivyo, itatathmini kiwango ambacho yanaweza kufikiwa kwa mfumo rahisi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA WAKALA WA MELI TANZANIA**

---

**JEDWALI LA KWANZA**

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(1)(iii))*

VIWANGO VYA UMWAGAJI MAJI TAKA KUTOKA KWENYE MELI

Viwango vilivyopendekezwa vinatengenezwa kwa mujibu wa azimio la IMO MEPC.157(55) lililopitishwa tarehe 13 Oktoba 2006 kama ilivyoainishwa hapa chini:

**1.0 UTANGULIZI**

1.1 Kanuni ya 5(1)(ii) na (iii) ya Kanuni hizi inatoa masharti kuwa maji taka ambayo hayajatibiwa, ambayo yanaweza kumwagwa kwa umbali wa zaidi ya maili 12 kutoka ardhi ya karibu, yasimwagwe mara moja bali kwa kiwango cha uondoshaji pale ambapo meli iko njiani na inaendelea kwa kasi isiyopungua fundo 4.

1.2 Kiwango hicho kitaidhinishwa na Shirika na kiwango kitatoa mwongozo wa uidhinishaji na ukokotoaji wa kiwango cha wastani cha kumwaga maji taka kinachotumika katika umwagaji wa maji taka ambayo hayajatibiwa na ambayo yamehifadhiwa kwenye matanki.

1.3 Viwango hivi havijumuishi kuzimuliwa maji taka au maji ya kijivu katika ukokotoaji wa uondoshaji maji taka au maji ya kijivu. Katika suala hili, kiwango hicho ni kiasi cha makadirio na inatambulika kuwa uondoshaji wa maji taka kwa mujibu wa Viwango hivi utatoa kiwango cha juu cha ulinzi kwa mazingira ya bahari kutokana na kuchanganya kabla ya uondoshaji pamoja na hatua ya kuchanganya kuamka kwa meli.

**2.0 FASILI**

2.1. "kiasi cha mafuta ambacho uondoshwa au kuhamishwa na pistoni inayosukumwa wakati wa kufungua au kufunga mzunguko." maana yake ni upana wa meli mara umbali kati ya njia ya maji na sehemu ndani kabisa ya boti mara umbali uliosafirishwa.

"maji taka yasiyotibiwa" maana yake ni maji taka ambayo hayaja-:

(a) tibiwa na aina iliyoidhinishwa ya kutibu maji taka; au
(b) punguzwa na kutibiwa

**3.0 KIWANGO CHA UTIRIRISHAJI**

3.1. Kiwango cha juu kinachoruhusiwa kutiririshwa ni 1/200,000 (au sehemu moja ya 200,000) ya ujazo kama ifuatavyo:

$DRmax = 0.00926\ V\ D\ B$

*Endapo:*

*DRmax ni kiwango cha juu kinachoruhusiwa kutiririshwa (m3 /h)*

*V ni kasi ya wastani ya meli (mafundo) katika kipindi hicho*

*D ni umbali wa kati yan jia yam aji na sehemu ya ndani kabisa ya boti (m)*

*B ni Upana(m)*

3.2. Kiwango cha juu kinachoruhusiwa cha kutiririshwa kilichobainishwa katika 3.1 kinarejea kiwango cha wastani kinachohesabiwa katika kipindi chochote cha saa ishirini nanne , au kipindi cha kutiririshwa ikiwa ni kidogo, na kinaweza kuzidishwa kwa si zaidi ya asilimia ishirini inapopimwa kwa kila saa.

**4.0 KIWANGO KILICHIIDHINISHWA NA SHIRIKA**

4.1. Shirika litaidhinisha kiwango cha utiririshaji kilichobainishwa katika 3.1 kulingana na umbali kati ya njia ya maji na sehemu ya ndani kabisa ya boti majira ya joto na kasi ya juu ya huduma. Tahadhari ya waendesha meli na wafanyakazi itazingatiwa kwa kupunguza kiwango kinachoruhusiwa cha utirirrishaji kwa umbali kati ya njia ya maji na sehemu ya ndani kabisa ya boti iliyopunguzwa na/au kasi.

4.2. Endapo maji taka yanapaswa kutiririshwa kwa mchanganyiko tofauti wa umbali kati ya njia ya maji na sehemu ya ndani kabisa ya boti na kasi moja au zaidi ya viwango vya utiririshaji wa pili vinavyoweza kuidhinishwa. Rejea Jedwali hapo chini:

| **KIWANGO CHA URIRISHAJI (m³/h)** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **SPIDI (kt)** | **4** | **6** | **8** | **10** | **12** |
| Umbali kati ya njia ya maji na sehemu ya ndani kabisa ya boti(m) | | | | | |
| 5 | 4.63 | 6.94 | 9.26 | 11.57 | 13.89 |
| 6 | 5.56 | 8.33 | 11.11 | 13.89 | 16.67 |
| 7 | 6.48 | 9.72 | 12.96 | 16.20 | 19.45 |
| 8 | 7.41 | 11.11 | 14.96 | 18.52 | 22.22 |
| 9 | 8.33 | 12.50 | 16.67 | 20.83 | 25.00 |

4.3. Kwa meli zaidi ya zile zenye mahitaji makubwa kwa maji machafu ambayo hayajatibiwa, kama vile meli za abiria na wabebaji wa mifugo, vigezo vya viwango vya utiririshaji havitazidi kasi ya meli ya noti 4.

**5.0 NJIA ZA UKOKOTOAJI**

5.1. Kiasi kilichokokotolewa cha kiasi cha mafuta ambacho uondolewa au kuhamishwa na pistoni inayosukumwa wakati wa kufungua au kufunga mzunguko kitabainishwa kwa umbali kati ya njia ya maji na sehemu ya ndani kabisa ya boti hadi na inajumuisha majira ya joto kwa mujibu wa Kanuni za Usafirishaji wa Wafanyabiashara (Laini ya Mzigo), TS. Na. 63 la 2019.

5.2. Endapo meli itatiririsha maji taka kutoka kwa tangi la kushikilia kwa kutumia pampu iliyosimikwa ya kudumu kwa kiwango kilichowekwa, pampu inaweza kusawazishwa:

(a) kwa kiwango kinachoruhusiwa kwa fundo 4; au

(b) kwa mwendo wa chini kabisa wa meli unaozidi mafundo 4

5.3. Endapo kiwango halisi cha utiririshaji kilichokusudiwa kinazidi kiwango kinachokubalika kwa noti 4, kiwango halisi cha utiririshaji kinaweza kuhitajika kupunguzwa au kasi kuongezwa. Kiwango na kasi kitaelezewa kwa kina katika idhini iliyotolewa na Shirika.

**6.0 UZINGATIAJI WA VIWANGO**

6.1. Kabla ya kutekeleza utiririshaji wa maji taka kwa mujibu wa Kiwango hiki, mfanyakazi anayehusika na shughuli za maji taka atahakikisha kuwa meli iko njiani, iko zaidi ya maili 12 kutoka ardhini iliyo karibu na kasi ya kusogeza inalingana na kiwango cha utiririshaji ambacho kilichoidhinishwa na Shirika. Meli zenya mahitaji makubwa ya utiririshaji zinahimizwa kuweka kumbukumbu za mahesabu ya utiririshaji halisi ili kuonyesha ufuatiliaji wa kiwango kilichoidhinishwa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA WAKALA WA MELI TANZANIA**

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1))*

VIPIMO SANIFU VYA MIUNGANISHO YA KUTIRIRISHA MAJI TAKA

| **Maelezo** | **Kipimo** |
|---|---|
| Kipenyo cha nje | *Kipenyo cha nje milimita 210* |
| Kipenyo cha ndani | *Kipenyo cha ndani Kulingana na kipenyo cha bomba nje* |
| Kipenyo cha komeo la mzunguko | *Kipenyo cha mduara wa bolt milimita 170* |
| Mpenyo wa kigingi | *Mpenyo katika mashimo manne, milimita kumi na nane kwa kipenyo, iliyowekwa kwa usawa kwenye mduara wa bolti wa kipenyo cha hapo juu, uliowekwa kwenye ukingo wa mpenyo. Upana wa kipenyo utakuwa milimita 18* |

| | |
|---|---|
| *Unene wa Mpenyo* | *milimita 16* |
| Mpenyo na nati: *kiasi na kipenyo vipande* | *4, kila moja ya milimita 16 katika kipenyo na urefu wa kufaa* 4 |
| Ukingo wa bapa umeundwa ili kukubali mabomba hadi kipenyo cha juu cha ndani cha milimita 100 na itakuwa ya chuma au nyenzo nyingine sawa na uso bapa. Ukingo huu, pamoja na gasketi inayofaa, itafaa kwa shinikizo la huduma ya kilopascal 600. | |

Kwa meli iliyo na kina cha mita 5 na chini, kipenyo cha ndani cha unganisho la kutiririsha kinaweza kuwa milimita 38.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA WAKALA WA MELI TANZANIA**

**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12(1))*

CHETI CHA KUZUIA UCHAFUZI UTOKANAO NA MAJI TAKA

Imetolewa chini ya masharti ya kanuni ya 12(1)
chini ya mamlaka ya Serikali ya.

...................................................................................................................
*(Jina kamili la nchi)*

na...............................................................................................................
*(Uteuzi kamili wa mtu au shirika linalofaa iliyoidhinishwa chini ya masharti ya Mkataba)*

**Maelezo ya meli:**

| Meli mpya ya abiria | Meli ya abiria iliyopo | Meli tofauti na meli ya abiria |
|---|---|---|
| | | |

Jina la Meli: ........................................................................................
Namba au Herufi pekee: ........................................................................................
Bandari ya Usajili: ........................................................................................
Ukubwa wa Jumla ya Tani: ........................................................................................
Namba ya Watu ambao wanaweza kubebwa na meli: ........................................................................................
Namba ya IMO: .............................................................................

**HII NI KUTHIBITISHA KWAMBA:**

1. Kwamba meli ina mtambo wa kusafisha maji taka/msimamizi/ tangi la kushikilia* na bomba la kutiririsha maji kwa kuzingatia Kanuni hizi:
1.1 Maelezo ya kituo cha kutibu ya maji taka:
1.2 Aina ya mtambo wa kutibu maji taka………………………….
1.3 Jina la mtengenezaji..............................................................
1.4 Kiwanda cha kusafisha maji taka kimeidhinishwa na Shirika ili kukidhi viwango vya maji taka kama ilivyoainishwa katika-
(a) azimio la MEPC.2(VI) kuhusu Mapendekezo ya Viwango vya Kimataifa vya

Maji Taka na Miongozo ya Uchunguzi wa Utendaji wa Mitambo ya Kusafisha Maji taka, 1976;

(b) azimio la MEPC.159(55) kuhusu miongozo iliyorekebishwa ya utekelezaji wa Viwango vya maji taka na Miongozo ya Uchunguzi wa Utendaji wa Mitambo ya Kusafisha Maji taka, 2006; na

(c) azimio la MEPC.227(64) kuhusu Mwongozo wa 2012 wa utekelezaji wa viwango vya maji taka na mtihani wa utendaji wa mitambo ya kusafisha maji taka.

* *futa yasiyo hitajika*

1.1. Maelezo ya msafiri:
Aina ya msafiri..................................................................
Jina la mtengenezaji ..............................................................
Kiwango cha maji taka baada ya kutibiwa .......................................

1.2. Jumla ya uwezo wa tangi la kushikilia..............................................$m^3$
Eneo..................................................................................

1.3. Bomba la kutiririsha maji taka kwenye kituo cha mapokezi, kilichounganishwa na unganisho la kawaida la pwani.

2. Kwamba meli imechunguzwa kwa mujibu wa kanuni ya 9 ya Kanuni hizi.

3. Kwamba uchunguzi unaonyesha kuwa muundo, vifaa, mifumo, vifaa, mipangilio, nyenzo za meli na hali yake ni ya kuridhisha kwa hali zote na kwamba meli inazingatia mahitaji ya Kanuni hizi

Cheti hiki kitakuwa halali mpaka...................................................... kwakuzingatia utafiti kwa mujibu wa kanuni ya 4 ya Kiambatisho cha IV cha Mkataba.

Tarehe ya kukamilika kwa uchunguzi ambao Cheti hiki kinategemea:
....................................................................
*(tarehe/mwezi/mwaka kilipotolewa)*
ni......................................................................
*(Mahali ambapo Cheti kimetolewa)*

....................... ………………………….……………………………………………

*(Tarehe ya kutolewa)* *(Saini ya afisa aliyeidhinishwa anayetoa Cheti)*

*(Seal or stamp of the authority, as appropriate)*

**Uidhinishaji wa kuongeza uhalali wa Cheti kwa kipindi kisichopungua miaka 5.**

Meli inafuata masharti husika ya Kanuni hizi, na Cheti hiki kitakubaliwa kuwa halali hadi:
………………..………
*(tarehe/mwezi/mwaka)*

..............................................
*(Saini ya afisa aliyeidhinishwa)*

Eneo: ....................................................... Tarehe:.....................................................................

*(Weka muhuri au muhuri wa mamlaka, inavyofaa)*

**Uidhinishaji iwapo uchunguzi mpya umekamilika na kanuni ya 9 ya Kanuni hizi.**
Meli imezingatia masharti husika ya Kanuni hizi na Cheti hiki kitakubaliwa kuwa halali hadi:
………………..………
*(tarehe/mwezi/mwaka)*
..............................................
*(Saini ya afisa aliyeidhinishwa)*
………………..………

Eneo: .................................................................... Tarehe:.............................................................. ..

*(Weka muhuri au muhuri wa mamlaka, inavyofaa)*

*Uidhinishaji wa kuongeza uhalali wa Cheti hadi kufikia bandari ya uchunguzi au kwa muda msamaha.*

Cheti hiki kwa mujibu wa kanuni ya 8.5 au 8.6 * ya Kiambatisho cha IV cha Mkataba, kitakubaliwa kuwa halali hadi:
………………..………
(*tarehe/mwezi/mwaka*)

..............................................
*(Saini ya afisa aliyeidhinishwa)*

** Futa inavyofaa*

Eneo: .................................................................... Tarehe: .....................................................................

*(Weka muhuri au muhuri wa mamlaka, pale panapofaa)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA WAKALA WA MELI TANZANIA**

____________

**JEDWALI LA NNE**

____________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12(2))*

CHETI CHA MSAMAHA WA MASHARTI YA KUZUIA UTIRIRISHAJI WA MAJITAKA BAHARINI KA KWA MASHUA ZISIZOJIENDESHA ZENYEWE

Imetolewa chini ya masharti ya kanuni ya 12 (2)
chini ya Mamlaka ya Serikali ya:

…………………………………………………………………………………………………………

*(Jina kamili la nchi)*

na ……………………………………………………………………………………………………

*(Jina kamili la mtu mwenye uwezo au shirika lililoidhinishwa chini ya masharti ya Mkataba)*

| | |
|---|---|
| **Maelezo ya meli:** | ……………………………………………..………………… …… |
| Jina la meli: | ……………………………………..………………………… …… |
| Namba au Herufi pekee: | ……………………………………..………………………… …… |
| Bandari ya Usajili: | ……………………………………..………………………… …… |
| Ukubwa wa Jumla ya Tani: | ……………………………………..………………………… …… |

**HII NI KUTHIBITISHA KWAMBA:**

1. Mashua zinazojiendesha imechunguzwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.
2. Uchunguzi unaonesha kuwa mashua inajiendesha:
   (a) haiendeshwi kwa njia za mitambo;
   (b) haina watu wala wanyama ndani ya ndege;
   (c) haitumiki kwa kuweka maji taka wakati wa kusafirisha; na
   (d) hana mipango inayoweza kuzalisha maji taka kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni hizi.

3. Kwamba mashua inayojiendesha imesamehewa, kutoka katika masharti ya uidhinishaji na uchunguzi chini ya Kanuni hizi

Cheti hiki ni halali hadi:

…………………………………………………………

(*tarehe/mwezi/mwaka*)

Kwakuzingatiamasharti ya msahama yanazingatiwa.
Tarehe ya kukamilika kwa utafiti ambao Cheti hiki kinazingatia

…………………………………………………………
(*tarehe/mwezi/mwaka*)

Kimetolewa ………………………………………………………………………………

*(mahali ambapo Cheti kimetolewa)*

| | |
|---|---|
| .................................................... | .......................................................... .. |
| *(tarehe kilipotolewa) (tarehe/mwezi/mwaka)* | *(saini ya afisa aliyeidhinishwa anayetoa Cheti)* |

*(muhuri au muhuri wa mamlaka, kadiri inavyofaa)*

Dodoma
3 Mei, 2024

MAKAME M MBARAWA
*Waziri wa Uchukuzi*